# IV.
# Financial Management

# Mada ya 40d

# Jinsi ya kuweka rekodi za bidhaa zilizomo dukani

# JARIDA LA UHAKIKA

## IV. Financial Management

## Mada ya 40d: Jinsi ya kuweka rekodi za bidhaa zilizomo dukani

1. **Bidhaa zilizomo dukani** ni pamoja na bidhaa zote **zilizonunuliwa au kuletwa na msambazaji.** Hizi huhifadhiwa na huweka mahali palipo rahisi kwa wateja kuona ili wazinunue. Kwa mfano, mwuzaji wa pembejeo za kilimo ataweka aina tofauti za mbolea, sumu ya magugu, sumu ya kuvu, viuawadudu, vifaa vya usalama, na vifaa vya kunyunyizia kama kinyunyizio cha shanta.
2. Ni muhimu kuweka **rekodi za bidhaa zilizomo dukani** kwa sababu hukujuza bidhaa zilizouzwa, kiasi kilichosalia, na kiasi kinachofaa kuagizwa au kununuliwa kwa wakati wowote ule. Itakusaidia kupanga vizuri lini utaagiza bidhaa mpya na kuepuka kuishiwa na bidhaa mara kwa mara au kuwa na bidhaa zilizopitisha muda wa mwisho wa matumizi.
3. **Rekodi za bidhaa zilizomo dukani** huwekwa kulingana na **kila bidhaa**, kwa hivyo kila bidhaa itakuwa na rekodi yake, na itaonyesha vifuatavyo:

| **Bidhaa za Ultracide – chupa za lita moja** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Bidhaa zilizomo wakati wa kufungua pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi** | **Kiasi kilichouzwa** | **Kiasi kilichonunuliwa** | **msambazaji** | **Bidhaa zilizomo wakati wa kufunga pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi** |
| 09 Jan 2009 | Feb 2010: 10<br>Mei 2010: 38 | 6 | | | Feb 2010: 4<br>Mei 2010: 38 |
| 10 Jan 2009 | Feb 2010: 4<br>Mei 2010: 38 | 1 | | | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38 |
| 11 Jan 2009 | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38 | | 50 | “Golden inputs” | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Desemba 2010: 50 |
| 14 Jan 2009 | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38<br>Desemba 2010: 50 | 4 | | | Mei 2010: 37<br>Decsemba 2010: 50 |

- Katika mstari wa juu, ingiza **jina la bidhaa** na **kiwango/kiasi** (lita, kilo)
- Tarehe: **tarehe ya kuingiza, pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi**
- Bidhaa zilizomo wakati wa kufungua: **ni kiasi gani kilikuwepo siku ilipoanza**
- Kiasi kilichouzwa**: ni kiasi gani kiliuzwa katika siku hiyo**
- Kiasi kilichonunuliwa: **ni kiasi gani kilinunuliwa kwa siku hiyo**
- **Msambazaji:** Jina la msambazaji
- **Bidhaa zilizomo wakati wa kufunga:** Ni kiasi gani kilichobakia mwishoni mwa siku, pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi

Kumbuka: bidhaa zilizomo wakati wa kufunga ndizo za kufungua siku ifuatayo.

➡ **Bidhaa zilizopitwa na wakati** ni zile ambazo haziwezi kuuzwa tena. Mfano ni kama bidhaa zilizopita tarehe ya mwisho wa matumizi. Pembejeo za kilimo haziwezi kuwekwa milele. Bidhaa zingine huharibika baada ya mwaka mmoja. Kwa jumla, **bidhaa zilizopita tarehe ya mwisho wa matumizi haziwezi kuuzwa**. Tarehe ya mwisho wa matumizi huandikwa kwenye bidhaa kwa wakati wowote.

➡ Njia nzuri ya kuepuka kuwa na bidhaa zilizopitwa na wakati ni kufuata **kanuni ya KKKK**: kwanza kuingia, kwanza kutoka. Bidhaa **zilizonunuliwa kwanza** (na zimekaa sana dukani) zinauzwa kwanza. Ni muhimu kwa wauza pembejeo za kilimo kwanza kuuza bidhaa ambazo tarehe ya mwisho wa matumizi iko karibu ikilinganishwa na bidhaa zingine. Katika mfano wa hapo juu, chupa nne ziliuzwa Jan 14, 2009. Katika siku hiyo, bidhaa zilikuwa na tarehe tatu tofauti za mwisho wa matumizi, (Februari 2010, Mei 2010, na Desemba 2010). Bidhaa zilizo na tarehe ya karibu ya mwisho wa matumizi ziliuzwa kwanza (chupa tatu za Februari 2010) halafu chupa moja ya Mei 2010 iliuzwa (jumla ya chupa nne). Ikiwa utaweka rekodi za bidhaa zako, tarehe za mwisho wa matumizi zitaingizwa kwenye rekodi na utajua bidhaa za kuuza kwanza.

# MAELEZO YA ZIADA

## IV. Financial Management

## <u>Mada ya 40d:</u> Jinsi ya kuweka rekodi za bidhaa zilizomo dukani

Kuchunguza bidhaa zinazoingia na kutoka (rekodi za bidhaa) kunaweza kuwekwa na kutengenezwa upya kila siku, mwezi, miezi mitatu au mwaka mzima.

Umbo la uwekaji rekodi hizi hutofautiana kidogo lakini bado hupeana habari inayohitajika kwa kufikia nambari sahihi kuhusu kuingia na kutoka kwa bidhaa. Uwekaji rekodi za bidhaa ni muhimu katika kufanya uamuzi na usimamizi wa biashara.

Rekodi za bidhaa pia husaidia kuamua mwelekeo wa biashara kwa wakati wote ule; huzidisha ubora wa udhibiti wa biashara. Rekodi husaidia kukagua makosa na ulaghai iwapo watu wawili au zaidi wanahusika katika shughuli za biashara za kila siku au usimamizi wa biashara.

Rekodi za bidhaa ni muhimu kwa kufanya uamuzi kuhusu sehemu za biashara au bidhaa ambazo zafaa kusisitizwa au kuacha kuuzwa. Kwa mfano, kama bidhaa hainunuliwi sana na inaendelea kuwa kwenye ghala, mwuzaji wa pembejeo za kilimo anaweza kuamua kutoweka bidhaa hii tena.

Bidhaa ni za sasa au nzee kulingana na tarehe ziliponunuliwa au kuwekwa kwenye ghala. Kwa mara Nyingi, **bidhaa za sasa** ni bidhaa mpya zikilinganishwa na zile zilizonunuliwa awali. **Bidhaa nzee** ni zile ambazo zimekaa kwenye ghala kwa muda unaopita mwaka mmoja.

# MWONGOZO

## IV. Financial Management

## Mada ya 40d: Jinsi ya kuweka rekodi za bidhaa zilizomo dukani

**Vifaa vinavyohitajika:**

- ☑ Ubao ulio na makaratasi
- ☑ Markers (1 nyeusi, 1 bluu, 1 kijani, 1 nyekundu)
- ☑ Copies for each participants of Visual 1 and Visual 2

**Muda unaohitajika:** Dakiki 75

**Maandalizi:**

- ☑ Chupa 12 tupu zilizo na "kibandiko": *viuawadudu, tarehe ya mwisho wa matumizi: Feb 2010*
- ☑ Chupa 8 tupu zilizo na "kibandiko": *viuawadudu, tarehe ya mwisho wa matumizi: Mei 2010*
- ☑ Makaratasi yaliochorwa fomu tupu
- ☑ Makaratasi yalio na maagizo yafuatayo:
  - Bidhaa zilizomo dukani wakati wa kufungua chupa 4 Juni 2010 na chupa 10 Agosti 2010
  - 8 Jan 2009 mauzo ya chupa 1
  - 10 Jan 2009 mauzo ya chupa 4
  - 11 Jan 2009 ununuzi wa chupa 50 kutoka kwa "Golden inputs", tarehe ya mwisho wa matumizi Desemba 2010

# Mwanzo

**U**sikivu: Uliza yeyote kueleza maana ya bidhaa zilizomo dukani. Ni pamoja na bidhaa zote zilizonunuliwa au kuletwa na

| | |
|---|---|
| | msambazaji na huweka mahali palipo rahisi kwa wateja kuona ili wazinunue. |
| **K**ichwa: | Waambie kwamba katika kipindi hiki utaeleza *jinsi ya kuweka rekodi za bidhaa zilizomo dukani* |
| **K**usadikika: | Eleza uzoefu wako katika uwekaji wa rekodi za bidhaa zilizomo dukani. |
| **M**alengo: | Kueleza jinsi ya kuweka rekodi za bidhaa zilizomo dukani. |
| **M**anufaa: | Ukiweka rekodi za bidhaa dukani, utapanga vizuri, na kuagiza bidhaa kwa njia bora ili kuepuka bidhaa kupitwa na wakati na pia utaepuka kupoteza pesa. |
| **M**welekeo: | Tutajadili tu rekodi za bidhaa zilizomo dukani, sio rekodi zingine. Kwa kuongezea, kanuni ya KKKK itaelezwa na sio kanuni zingine. |

# Wasilisho

## **U**fafanuzi, **M**aonyesho, **M**azoezi, na **M**wongozo:

1. Ambia washiriki kwamba tutaanza na **kanuni ya KKKK**. Uliza maana yake. Inasimamia; kwanza kuingia, kwanza kutoka. Inamaanisha kwamba bidhaa zilizonunuliwa kwanza (na zimekaa sana dukani) zinauzwa kwanza. Ni muhimu kwa wauza pembejeo za kilimo kwanza kuuza bidhaa ambazo tarehe ya mwisho wa matumizi iko karibu ikilinganishwa na bidhaa zingine.
2. Gawanya washiriki katika vikundi vinne na uvipatie chupa zifuatazo: chupa tatu zilizo na "kibandiko": *viuawadudu, tarehe ya mwisho wa matumizi Feb 2010*, na chupa mbili na "kibandiko": *viuawadudu, tarehe ya mwisho wa matumizi Mei 2010*. Waambie kwamba hizi chupa ndizo bidhaa za biashara yao. Mteja anaingia dukani na angependa kununua chupa mbili za viuawadudu. Ni chupa gani utauza kuambatana na kanuni za KKKK? Vikundi vijadili majibu.
3. Uliza kikundi kimoja kupeana jibu lao na uulize vikundi vingine kama vinakubaliana nacho. Jibu ni: utauza chupa mbili zilizo na tarehe ya mwisho wa matumizi ya Februari 2010. Kila kikundi kitoe chupa mbili zilizo na tarehe hiyo. Sasa kila kikundi kitakuwa na chupa moja ilio na tarehe ya mwisho wa matumizi ya Februari 2010 na chupa mbili zilizo na tarehe ya mwisho wa matumizi ya Mei 2010.
4. Waambie kwamba mteja mwingine anakuja dukani na angependa kununua chupa mbili pia. Ni chupa zipi utauza kuambatana na kanuni ya KKKK? Vikundi vijadili jibu.
5. Uliza kikundi kimoja kikupatie jibu na uulize kama vingine vinakubaliana. Jibu ni: utauza chupa moja ilio na tarehe ya mwisho wa matumizi ya Februari 2010, na ile ya Mei 2010.
6. Uliza kama kila mtu anaelewa kanuni ya KKKK.

7. Endelea na kusambaza picha ya 1. Eleza kwamba kwa kila bidhaa, utaweka rekodi tofauti. Jadili aina ya habari ya kuingizwa kwenye rekodi. Katika mstari wa juu, ingiza **jina la bidhaa** na **kiwango/kiasi** (lita, kilo).

   - **Tarehe**: tarehe ya kuingiza, pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi.
   - **Bidhaa zilizomo wakati wa kufungua**: ni kiasi gani kilikuwepo siku ilipoanza.
   - **Kiasi kilichouzwa**: ni kiasi gani kiliuzwa katika siku hiyo.
   - **Kiasi kilichonunuliwa**: ni kiasi gani kilinunuliwa kwa siku hiyo.
   - **Msambazaji**: Jina la msambazaji.
   - **Bidhaa zilizomo wakati wa kufunga**: Ni kiasi gani kilichobakia mwishoni mwa siku, pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi.

| **Bidhaa za Ultracide – chupa za lita moja** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Bidhaa zilizomo wakati wa kufungua pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi** | **Kiasi kilichouzwa** | **Kiasi kilichonunuliwa** | **msambazaji** | **Bidhaa zilizomo wakati wa kufunga pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi** |
| 09 Jan 2009 | Feb 2010: 10<br>Mei 2010: 38 | 6 | | | Feb 2010: 4<br>Mei 2010: 38 |
| 10 Jan 2009 | Feb 2010: 4<br>Mei 2010: 38 | 1 | | | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38 |
| 11 Jan 2009 | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38 | | 50 | "Golden inputs" | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38<br>Desemba 2010: 50 |
| 14 Jan 2009 | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38<br>Desemba 2010: 50 | 4 | | | Mei 2010: 37<br>Desemba 2010: 50 |

8. Uliza maswali yafuatayo:

   a. Ni bidhaa gani ya rekodi hizi? Ultracide, chupa za lita moja
   b. Ni nini kilifanyika Januari 11? Chupa 50 zilinunuliwa
   c. Ni bidhaa ngapi ziliuzwa Januari 10? Chupa moja
   d. Ni chupa ngapi tulizo nazo kwa jumla dukani tarehe ya Januari 14 mwishoni mwa siku hiyo? 87

9. Tazama vizuri chupa nne zilizouzwa Januari 14. Chupa tatu zilikuwa na tarehe ya mwisho wa matumizi ya Februari 2010 na chupa moja Mei 2010. Uliza ni kanuni gani iliotumiwa hapa. Ni kanuni ya KKKK (kwanza kuingia, kwanza kutoka).
10. Sambaza picha ya 2. Pamoja tutaingiza habari kutumia mfano. Onyesha karatasi *rekodi za bidhaa zilizomo dukani* lililo na habari ambayo utaingiza kwenye rekodi. Soma vitomeo vyote na uwaambie kuingiza habari hii katika rekodi zao za bidhaa zilizomo dukani:
    - Bidhaa za kufungua: chupa 4 June 2010 na chupa 10 Agosti 2010
    - 8 Jan 2009 mauzo ya chupa 1
    - 10 Jan 2009 mauzo ya chupa 4
    - 11 Jan 2009 ununuzi wa chupa 25 kutoka kwa "Golden inputs", tarehe ya mwisho wa matumizi Desemba 2010

    Watembelee ili kuona kama yeyote ana tatizo la kusuluhisha.
11. Onyesha karatasi lililo na rekodi tupu za bidhaa zilizomo dukani. Uliza wa kujitolea kuingiza kitomeo cha kwanza. Uliza kama kila mtu anakubaliana. Kariri kilichoingizwa, ili kila mtu asikie vizuri. Uliza wa kujitolea wa pili kuingiza habari ya pili, n.k.
12. Matokeo yafaa yawe ifuatavyo:

| **Bidhaa za Ultracide – chupa za lita moja** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Bidhaa zilizomo wakati wa kufungua pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi** | **Kiasi kilichouzwa** | **Kiasi kilichonunuliwa** | **msambazaji** | **Bidhaa zilizomo wakati wa kufunga pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi** |
| 08 Jan 2009 | Juni 2010: 4<br>Agosti 2010: 10 | 1 | | | Juni 2010: 3<br>Agosti 2010: 10 |
| 10 Jan 2009 | Juni 2010: 3<br>Agosti 2010: 10 | 4 | | | Agosti 2010: 9 |
| 11 Jan 2009 | Agosti 2010: 9 | | 25 | "Golden inputs" | Agosti 2010: 9<br>Desemba 2010: 25 |

# Malizia

**M**uhtasari: Tumia makaratasi yalio na fomu zilizokamilishwa kupeana muhtasari. Rudia aina ya habari inayofaa kuingizwa katika fomu hizo. Eleza kanuni ya KKKK.

**M**aswali: Uliza kama kuna yeyote aliye na swali au maoni.

**T**athmini: Pindua makaratasi na uulize kanuni ya KKKK. Kwanza kuingia, kwanza kutoka. Uliza ni kwa nini tutumie kanuni ya KKKK. Jibu ni kuepuka bidhaa kupitwa na wakati. Uliza aina ya habari inayofaa kuingizwa katika rekodi za bidhaa zilizomo dukani.

**H**atua fuatilizi: Hata kama hauna rekodi za bidhaa zilizomo dukani, unaweza kuanza kutumia kanuni ya KKKK sasa hivi.

Sambaza **makaratasi ya taarifa ya maelezo** kwa washiriki wote.

# VISUAL 1

## EXAMPLE RECORDS ON STOCK

| **Bidhaa za Ultracide – chupa za lita moja** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Bidhaa zilizomo wakati wa kufungua pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi** | **Kiasi kilichouzwa** | **Kiasi kilichonunuliwa** | **msambazaji** | **Bidhaa zilizomo wakati wa kufunga pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi** |
| 09 Jan 2009 | Feb 2010: 10<br>Mei 2010: 38 | 6 | | | Feb 2010: 4<br>Mei 2010: 38 |
| 10 Jan 2009 | Feb 2010: 4<br>Mei 2010: 38 | 1 | | | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38 |
| 11 Jan 2009 | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38 | | 50 | “Golden inputs” | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Desemba 2010: 50 |
| 14 Jan 2009 | Feb 2010: 3<br>Mei 2010: 38<br>Desemba 2010: 50 | 4 | | | Mei 2010: 37<br>Decsemba 2010: 50 |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

IFDC

# VISUAL 2

## EMPTY RECORDS ON STOCK

| Bidhaa za Ultracide – chupa za lita moja | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Tarehe | Bidhaa zilizomo wakati wa kufungua pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi | Kiasi kilichouzwa | Kiasi kilichonunuliwa | msambazaji | Bidhaa zilizomo wakati wa kufunga pamoja na tarehe ya mwisho wa matumizi |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

IFDC